TANGAZO LA SERIKALI Na. 238 la tarehe 4/4/2025

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA,
(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 16(1))*

## SHERIA NDOGO YA MAREKEBISHO YA SHERIA NDOGO YA USHURU WA MADINI YA UJENZI YA HALMASHAURI YA WILAYA YA PANGANI YA MWAKA 2025

Jina

TS Na. 792 la 2024

**1**. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Marekebisho ya Sheria Ndogo ya Ushuru wa Madini ya Ujenzi ya Halmashauri ya Wilaya ya Pangani ya Mwaka 2025, na itasomwa pamoja na Sheria Ndogo ya Ushuru wa Madini ya Ujenzi ya Halmashauri ya Wilaya ya Pangani ya Mwaka 2024 ambayo hapa imerejewa kama "Sheria Ndogo kuu".

Marekebisho ya kanuni ya 6

**2**. Sheria Ndogo kuu inarekebishwa katika kanuni ya 6 kwa kufuta na kuandika upya kanuni ndogo ya (2) kama ifuatavyo:

"(2) Kabla ya kufunga machimbo yoyote, Halmashauri itatakiwa kutoa notisi ya siku saba ya kusudio la kufunga machimbo kwa wakazi wa Halmashauri.".

Marekebisho kanuni ya 14

**3**. Sheria Ndogo kuu inarekebishwa katika kanuni ya 14 kwa kuongeza kanuni ndogo ya (5) kama ifuatavyo:

"(5) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (4), adhabu ya kufutwa au kusimamishwa kwa kibali itadumu kwa muda wa mwezi mmoja tangu ilipotolewa na baada ya hapo utaratibu wa kuomba kibali upya utapaswa kufuatwa.".

Dodoma
12 Machi, 2025

MOHAMED OMARY MCHENGERWA,
*Waziri wa Nchi- OR-TAMISEMI*